

102/3

KISWAHILI  
KARATASI YA TATU  
FASIH  
JULY / AUGUST 2010  
MUDA: SAA 2 ½

**MUUNGANO WA SHULE MBALIMBALI WILAYA  
YA KAKAMEGA KAZIKAZINI  
MTIHANI WA KUJITATHIMINI  
Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E) 2010**

102/3  
KISWAHILI  
FASIH  
JULAI / AGOSTI 2010

**MAAGIZO**

- ❖ *Jibu maswali manne pekee.*
- ❖ *Swali la kwanza ni la lazima.*
- ❖ *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki. Yaani (Riwaya, hadithi fupi, ushairi na Fasihi simulizi)*
- ❖ *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**TAMTHLIA**

**Kithaka wa Mberia : Kifo Kisimani**

1. **Eleza** sifa na umuhimu wa wahusika wafuatao katika tamthlia ya kifo kisimani

- (a) Mwelusi
- (b) Bokono
- (c) Batu

## **RIWAYA**

### **Jibu swali la 2 au 3.**

#### **Said A. Mohamed : UTENGANO**

2. Riwaya ya utengano inabainisha wazi maovu yanayoikumba jamii. **Thibitisha** kauli hii kwa kutoa mifano kumi. (alama 20)
3. ...na sasa matarajio ya Uhuru...  
...bado Afrika inatawaliwa...  
...inatawaliwa kwa mlango wa nyuma...
  - (a) **Fafanua** muktadha wa maneno haya (alama 4)
  - (b) **Eleza** sifa za msemaji wa maneno haya (alama 4)
  - (c) Wakati wa kisa hiki, msemaji na msemewa wanasababisha aina fulani ya ‘Utengano’ **taja** utengano huu na ueleze sababu zake. (alama 4)
  - (d) **Thibitisha** madai kwamba uhuru wa wahusika fulani katika riwaya hii haujatimia (alama 8)

## **HADITHI FUPI**

### **K. W. WAMITILA: Mayai Waziri wa maradhi na Hadithi nyingine**

#### **Jibu swali la 4 au 5.**

4. Mwanamume amesawiriwa vipi katika hadithi zifuatazo?
  - (a) Ngome ya nafsi
  - (b) Kachukua hatua nyingine
  - (c) Mayai waziri wa maradhi
  - (d) Uteuzi wa moyoni (alama 20)

## **Fumbo la mwana**

5. “.....Si nyinyi ndinyi mnaoshinda naye shulen?”
  - (a) **Eleza** muktadha wa dondo hili. (alama 4)
  - (b) **Taja** sababu zozote sita zinazothibitisha kuwa hadithi hii ni fumbo la mwana (alama 6)
  - (c) **Fafanua** sifa zozote nne za msemaji wa maneno haya. (alama 4)
  - (d) Dawa za kulevyaa zina athari gani kwa jamii? (alama 6)

## FASIHI SIMULIZI

6. (a) (i) **Taja** mbinu zozote tatu za kuhifadhi fasihi simulizi (alama 3)  
(ii) Taja aina zozote tatu za vitendawili (alama 3)  
(iii) Bainisha matumizi ya lugha katika vitendawili (alama 3)
- (b) (i) Ngomezi ni nini? (alama 1)  
(ii) Eleza ujumbe uliowasilishwa na ngomezi katika fasihi simulizi. (alama 3)  
(iii) Fafanua sifa zozote nne za ngomezi. (alama 4)  
(iv) Taja mifano mitatu ya ngomezi ya kisasa. (alama 3)

7. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Unganambia ni mui, katu siuwati wema,  
Wewe ndiwe wangu bui, nalousiwa ni mama,  
Leo kwamba siujui, ni kupotosha heshima,  
Siasi kutenda wema, kaandama uadui.

Wema nambiwa na ndia, hadi bandari salama,  
Hayo niliyasikia, nao wahenga wa zama,  
Penye wema tajitia, nipate taadhima,  
Siasi kutenda wema, japo munganinunia.

Ni iwe kupawa mali, ya kuhadaa mtima,  
Niandame ufidhuli, nitengane nao wema,  
Hilo sitokubali, japo waja wangasema,  
Siasi kutenda wema, ujapokuwa ni ghali.

Sitomcha kabaila, nganitenza nache wema,  
Munganitia na jela, kisa imefanza huruma,  
Haragwe lenu talila, pamoja na yenu sima,  
Siasi kutenda wema, japo tagoni talala.

Haufi mungaufisha, auhamipo Karima,  
Mola atauhuisha, welekeapo kuzama,  
Mimi ni huo maisha, hadi siku ya kiama,  
Siasi kutenda wema, nganitia mshawasha.

Wema ungawa mchungu, tajaribu kutotema,

Tautenda nende zangu, niache wanaosema,  
 Malipo yangu kwa Mungu, hayo yenu si lazima,  
 Siasi kutenda mema, kigharimu roho yangu.

- (a) Ukizingatia beti nne za mwanzo, **taja** mambo ambayo hata mshairi akifanyiwa hawezi kuacha  
kutenda mema. (alama 4)
- (b) **Eleza** jinsi mtunzi wa shairi hili alivyotumia uhuru wake. (alama 4)
- (c) Mshairi alipata wapi ari ya kuzingatia wema? (alama 1)
- (d) **Eleza** muundo wa ubeti wa pili ukizingatia mizani na vina. (alama 2)
- (e) **Eleza** maudhui ya shairi hili. (alama 2)
- (f) **Andika** ubeti wa mwisho katika lugha nathari. (alama 4)
- (g) **Eleza** maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi.
  - (i) Mtima
  - (ii) Kutotema
  - (iii) Kigharimu roho yangu (alama 3)